# LARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE THIRTEEN: “Under the Radar”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: CHIVASI TELLS HIS STORY TO THE IMMIGRATION OFFICER**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Immigration official (m, 40)**

**SCENE TWO: LINDA, CHARLES AND FLORENCE CELEBRATE AT THE NIGHTCLUB**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Charles (m, 45)**
- **Policeman (m, 35)**
- **3-5 guests (mixed gender, age not important)**

**SCENE THREE: CHIVASI ESCAPES FROM THE DETENTION CENTRE**

- **Farahani (m, 19)**
- **Chivasi (m, 22)**
- **Rhoda (f, 25)**

**INTRO:**

Hujambo msikilizaji na kwa mara nyingi karibu kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako. Hii ni sehemu ya 13 kuhusu uhamiaji mambo leo wa Wa-afrika kuelekea Ulaya kwenye hadithi **“ Ardhi ya Ahadi”.** Tumekuwa tukifuatilia maisha ya Linda, Farahani na Chivasi na tumefahamu kwamba ingawa Ulaya kunamaisha mazuri, elimu bora na nafasi nzuri za kujiendeleza maisha, bado kuna changamoto nyingi hasa kwa wahamiaji wasio halali.Katika kipindi kilichotangulia Linda anashtuka kusikia kwamba mume aliyefunga naye Ndoa bandia ili kupata kibali cha kufanya kazi Ulaya, ni mume wa zamani wa rafiki yake Florence. Na kwamba wawili hao ndio wamiliki wa klabu alikotafutiwa kazi na rafiki yake mkubwa Florence. Na anafikiria kuwacha masomo kwa muda ili aweze kufanya kazi wakati wote kupata pesa anazohitaji kwa dharura kugharamia matibabu ya Babake. Na katika kizuizi cha wahamiaji wasiohalali maafisa wa uhamiaji wameanza kuwahoji wahamiaji hao kwa lengo la kuwapa hifadhi ya wakimbizi. Wa kwanza kuhojiwa ni Farahani huku Chivasi akiwa wa mwisho kuhojiwa. Je! watafanikiwa kupata hifadhi ya Ukimbizi Ulaya? Endelea kuwa nasi katika sehemu ya mchezo huu **“Chini ya uchunguzi.”** Hebu sasa tuungane na Chivasi anapopambana na maafisa hao wa uhamiaji.

**SCENE ONE: CHIVASI TELLS HIS STORY TO THE IMMIGRATION OFFICIAL**

1. **SFX: PAPER FILE BEING OPENED**

2. **IMM. OFFICER:** Kwa hiyo wewe ndio, mpinzani mkubwa wa shetani.

3. **CHIVASI:** Mpinzani wahetani? Sikuelewi.Unamaanisha nini afande?

4. **IMM. OFFICER:** Ulijificha kwenye meli iliyokuwa ikileta chakula cha msaada Afrika na kuingia Ulaya kisiri kama mdandia Meli. Sikumbuki ni lini mara ya mwisho kumhoji mtu aliyefanya kosa kama hili lako. Kwa hiyo wewe ni shujaa, sivyo?

5. **CHIVASI:** Hapana afande. Nafikiri hiki ndicho kisa cha hatari zaidi kuwahi kufanya maishani mwangu.

6. **IMM. OFFICER:** Unahakika? Kwanini ukafanya hivyo? Kudandia meli hadi Ulaya bila ya kuonekana, umejaribu!.Hii ni tofauti kabisa na wahamiaji wengine wanaoingia Ulaya kisiri kwa kutumia mashua ndogo. Bila shaka safari yako ilikuwa yenye raha mstarehe. Una pesa zozote?

7. **CHIVASI:** **(perplexed)** Pesa? Yaani pesa katika sarafu ya Yuro?

8. **IMM. OFFICER:** Hata si Yuro tu – pesa zozote. Uko nazo?

9. **CHIVASI:** **(hesitant)** Ah… ndio… ahhh, nimezitumia...Niko na pesa kidogo,.. ndiyo Lakini si nyingi,.. lazima nisaidie familia yangu ambayo ni kubwa sana.

**10. IMM. OFFICER:** Uko na familia? Umeoa? Una watoto?

**11. CHIVASI:** Hapana sijaoa. Niko na mchu--…Niko na kaka na Dada .

**12. IMM. OFFICER:** Familia na mchumba sivyo. Heee? Wewe hufai kupewa hifadhi kama mkimbizi. Kwanini unatafuta hifadhi

**13. CHIVASI:** Kuliandaliwa uchaguzi nchini mwangu, lakini baada ya uchaguzi, ghasia za kikabila zikazuka. Nilitoroka ghasia hizo kwasababu zilikuwa zinawalenga watu kutoka kabila langu.

**14. SFX: SCRIBBLING ON PIECE OF PAPER**

**15. IMM. OFFICER:** Aha**…** Na je Familia yako? Maisha yao si yamo hatarini zaidi pia?

**16. CHIVASI:** Hapana – ahh ndiyo, Na hofia sana maisha yao!. Lakini najua wako salama

**17. IMM. OFFICER:** Unajuaje kwa hakika?

**18. CHIVASI:** Nauaje? Niliwaona.

**19. IMM. OFFICER:** Kabla ya kufunga safari kuja ulaya?

**20. CHIVASI:** Ndiyo.

**21. IMM. OFFICER:** Sawa…..kwa hivyo unasema baada ya uchaguzi

kulikuwa na ghasia za kidini - kwanini?

**22. CHIVASI:** Ah… kwa hakika sijui. Kila mara tumekuwa na tatizo hili.

**23. IMM. OFFICER:** Tatizo gani? Sielewi.

**24. CHIVASI:** Tatizo hili la ghasia za kidini.

**25. IMM. OFFICER:** Nafikiri umesema ghasia za kikabila .

**26. CHIVASI:** Kikabila ? Ah - ndiyo, ghasia za kikabila na kidini

**27. SFX: PEN DROPPED DOWN ON TABLE**

**28. IMM. OFFICER:** Ahsante. Hiyo inatosha kwa leo. Lakini samahani sana, sidhani kama sababu ulizotoa zinatosha kupewa hifadhi ya Ukimbizi.Unajikanganya sana na yaonekana unasababu nyingine za kuja Ulaya kinyume cha sheria. Kwa hivyo nimekataa ombi lako na utarejeshwa nyumbani haraka iwezekanavyo.

**29. CHIVASI:** Lakini… ni… kwanini ? Nimewaeleza kila kitu -

**30. IMM. OFFICER:** **(cuts him short)** Hiyo inatosha kwa sasa!.

**31. NARRATOR:** Chivasi hakuwa na jingine ila kuondoka pole pole kurudi katika chumba chake anakozuiliwa. Ameanguka mtihani na sasa

anasubiri kurejeshwa nyumbani rasmi.Je atakubaliana na hatua hiyo.? Kwa upande wake, Linda, Florence na Charles wanapumzika kwenye klabu…

**SCENE TWO: LINDA, CHARLES AND FLORENCE AT NIGHTCLUB**

**32. SFX: MUSIC PLAYING IN BACKGROUND**

**33. FLORENCE:** Babako anaendeleaje, Linda? Umepata habari zozote?

**34. LINDA:** Ndiyo! madaktari walifanikiwa akumfanyiwa operesheni. Wanasema sasa anaendelea vizuri.

**35. FLORENCE:** Ukiacha masomo yako kwa muda na kufanya kazi siku zote, mambo yatabadilika. Na muda si mrefu idara ya uhamiaji itakupatia kibali cha uraia na utaweza kufanya unavyotaka!

**36. LINDA:** Bado siamini! Hiyo ni kama ndoto tu.

**37. SFX: POLICE SIRENS FROM OUTSIDE GETTING LOUDER**

**38. POLICEMAN:** **(screams from afar)** Sisi ni maafisa wa polisi! Kila mmoja atulie mahali alipo!

**39. SFX SOME GUESTS PANIC, MUSIC IS TURNED OFF**

**40. POLICEMAN:** Wewe ni Florence sivyo?. Na huyu ni mumeo wa zamani, Charles, sivyo?, Nyinyi ndio wamiliki wa klabu hii?

**41. CHARLES:** Ndiyo

**42. POLICEMAN:** Na huyu msichana bila shaka ni Linda Maraga.Mwanafunzi wa chuo kikuu ambaye sasa ameolewa na Charles. Sivyo?

**43. FLORENCE:** Ndiyo.Kuna tatizo Ofisa?

**44. POLICEMAN:** Tumekuwa tukifuatilia sana mienendo yenu kwa muda mrefu. Na sasa mko chini ya ulinzi wa polisi kwa kuhusika na njama ya kupanga ndoa bandia baina ya Waafrica na Wazungu kwa madhumuni ya kuwasaidia kupata vibali vya uraia Ulaya, na kisha kuwalazimisha kufanya kazi katika klabu yenu. Hivyo kuwanyima haki zao za kimsingi. Pindi itakapobainika kwamba kunaushahidi wa kutosha kuhusu madai ya ndoa bandia baina ya Linda na Charles, basi ndoa hiyo itafutiliwa mbali na mahakama. Na wewe Bi Maraga…. Hatujui kama ulilazimisha kwenye sakati hii au ni ulifanya kwa mapenzi yako. Bado haijabainika kwa hivyo uko huru kuendelea na shughuli zako hadi pale kutakuwa na ushahidi wa kutosha kukuhusisha na sakata hii.

**45. CHARLES:** **(very scared)** Ofisa! Kwa hakika sielewi

mnazungumzia nini?.Labda umekosea!.

**46. FLORENCE:** **(cool)** Charles, tulia usiwe na wasi wasi. Bado haya ni madai ambayo hayajathibitishwa. Hatuna hatia hadi pale itakapothibitishwa kwa hakika tunamakosa. Sioni ushahidi wowote hapa kuonyesha tumefanya kosa. Kwa hiyo tufuate maagizo ya mafisa wa polisi na kuandamana nao.

**47. SFX: HANDCUFFS BEING USED TO CUFF HANDS**

**48. NARRATOR:** Linda anatazama kwa hofu huku Florence na Charles wakitiwa pingu na kuongozana nje ya klabu na maafisa hao wa Polisi. Je Florence na Charles watapatikana na hatia? Na Linda atafanya nini? Tusikilize yatakayojiri. Kwengineko katika kuzuizu cha wahamiaji bandia, Chivasi anatoa siri zake kwa Farahani, ambaye anaamini baada ya mahojiano yake atapewa hifadhi kama mkimbizi. Farahani naye anampa siri Chivasi ya atakavyofanya baadaye kubakia Ulaya.…

**SCENE THREE: CHIVASI ESCAPES FROM THE DETENTION CENTRE**

**49. FARAHANI:** Una uhakika amekwambia hutapewa hifadhi?

**50. CHIVASI:** Ndiyo ameniambia hivyo kwamba haniamini!. Amesema kuwa nimejikanganya sana na katika muda wa siku chache zijazo nitarudishwa nyumbani.

**51. FARAHANI:** Unataka hivyo? Kurudi nyumbani Afrika?

Kwasababu kama kweli unataka kuendelea kuishi Ulaya, ipo njia moja tu iliyosalia.

**52. CHIVASI:** Gani hiyo? Ni njia gani hiyo? Nimetoka safari yote hiyo... na lazima nitimize ndoto yangu, kwa vyovyote vile nimuone Linda. Sasa nifanyaje?

**53. FARAHANI:** Sasa hutapewa hifadhi, kwa hiyo lazima ujifiche chini ya Rada .

**54. CHIVASI:** Chini ya Rada ? yaani nisionekane?

**55. FARAHANI:** Hasa! Utakuwa unahatarishamaisha yako. Namfahamu mtu ambaye anarafiki yake akimwambia nimekutuma atakusaidia. Lakini lazima kwanza utoroke hapa kizuizini. Nimekuwa nikifikiria sana jambo hilo endapo ombi langu litakataliwa. Sikiliza hapa…

**56. NARRATOR:** Haraka haraka Farahani anamuarifu Chivasi atakavyo fanya. Baada ya muda mchache gari la mizigo linawasili na tayari Chivasi anasubiri nje ya jengo kuu ndani ya kambi hiyo ya kuzuizi. Na wakati dereva anapotazama upande mwengine, Chivasi anabingiria chini ya gari hilo na kujishikilia vizuri chini ya gari hilo kwa nguvu zake zote. Kisha gari hilo linatoka nje na kuanza safari ya kuelekea mjini kupitia badrabara kuu kwa kasi.…

**57. SFX: VAN SPEEDING DOWN THE STREET**

**58. CHIVASI:** **(cursing)** Kwanini nikaamua kuja huku? Huu ni wazimu! Nilikuwa na kila kitu ninachohitaji nyumbani. Aaaah … Linda, natumaini unanisubiri. Nitaungana nawe hivi punde. Uuuuh! Taabu hizi zote kwasababu yako! Nimechoka siwezi kujizuia tena.…

**59. SFX: VAN SLOWS AND STOPS AT A TRAFFIC LIGHT**

**60. CHIVASI:** Leo ni leo msema kesho ni muongo! **(lets go)**

**61. SFX: SOMEONE FALLING WITH A THUDDING SOUND / STREET ATMO**

**62. CHIVASI:** Oooohowwwww – Mgongo wangu! Auuuuh…Mgongo wangu!

**63. RHODA:** **(concerned)** Umeumia? Ohhh – unatokwa na damu! Tuite haraka gari la wagonjwa! Subiri kwani unakwenda wapi?

**64. CHIVASI:** **(in pain)** Hakuna haja ya kuitisha Ambulensi, wala polisi niko sawa tafadhali!. – Hili ndilo jiji? Unaweza kunionyesha njia ya kuelekea chuo kikuu?

**65. RHODA:** Jiji ? hapana,- ni mbali sana!,. Sikiliza naitwa Rhoda, naishi hapa karibu tu!. Kwani usiandamane nami hadi kwangu kama hutaki kwenda hospitalini? Naweza kukupatia huduma ya kwanza kisha

uendelee na safari yako.

**66. CHIVASI:** Asante sana. Auuuuh! Pole pole tafadhali …asante sana…

**67. RHODA:** Twende huku, hebu nifuate..

**68. CHIVASI:** **(confused)** Nataka kwenda. Nimechelewa!.

**69. RHODA:** Ukiwa katika hali hii! Unavuja damu na unahitaji maji moto na chakula. Hebu nifuate tafadhali. Najua unapitia hali ngumu sana. Sitakudhuru.Mimi ni msamaria mwema tu.

**70. SFX: POLICE SIRENS FROM AFAR**

**71. CHIVASI:** **(scared)** Ohh tumechelewa Polisi wamefika!

**72. RHODA:** Usiwe na wasi wasi! Nishike Mkono. Sasa tutembee pamoja. Sawa,…. twende huku.…!

OUTRO:

Je Chivasi atafanikiwa kukwepa maafisa wa Polisi? Na hata akifanikiwa bado hana pesa wala stakabadhi zozote.- Ni vipi ataweza kumtafuta Linda? Na je Frahani anaendeleaje?. Na Iwapo ombi lake litakubaliwa na kupewa hifadhi, hii inamaana shida zake zitakuwa zimekwisha? Ungana nasi kwa kipindi kinachofuata upate jawabu la maswali haya yote kwenye sehemu ya 14 ya mchezo huu**“Ardhi ya ahadi”**. Lakini kwa sasa tunakualika kuchangia hoja zake kuhusu maisha yaloivyo kwa wahamiaji wasio halali na pia maisha chini ya Rada. Pia endapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea

mtandao wetu wa dw-de/destinationeurope. Hadi wakati mwengine kwaheri.